

A Sheria na imani. Warumi 3:31.

- ❖ Kama Warumi 3:31 inavyoeleza, inami na sheria havitenganishi. Imani huithibitisha sheria.
- ❖ **Imani ya Ibrahimu. Warumi 4:1-5.**
 - Ibrahimu alipokea haki kwa Imani na si kwa matendo. Bado alikuwa mmataifa asiyetahiriwa alipookolewa (maana Israeli haikuwepo bado).
 - Hii iliwachanganya waliofikiri kuwa wakristo wanapaswa kuwa wayahudi ili waokolewe.
- ❖ **Imani ya Daudi. Warumi 4:6-8.**
 - Daudi angewezaje kuwa huru dhidi ya dhambi yake?
 - Kama angefikiri kuwa anahesabiwa haki kwa matendo, angejitesa. Pengine angefanya safari nyngi za hija au kutoa kafara maelfu ya wanyama.
 - Alijua kuwa Mungu pekee anaweza kumsamehe kwa neema pekee.

B Kazi ya sheria.

- ❖ **Sheria na ahadi. Warumi 4:9-17.**
- ❖ Kwa kuwa Ibrahimu aliahidiwa wokovu kabla ya sheria, angeweza kuokolewa kwa Imani pekee. Sheria haikuhusika katika wokovu wake
- ❖ **Sheria na wokovu. Galatians 3:21-23.**
 - Dini zisizo za kikristo hufundisha kuwa tunaweza kupata uzima wa milele kwa kufanya jambo fulani (Kuhiji, kutafakari, kujitoa kafara...)
 - Dini ya kiyahudi hukumbatia dhana ya kutimiza sheria kwa usahihi...)
 - Hata kanisa la kikristo lilifuata kosa hilo. Lakini Luther na wanamatengenezo wengine walirejesha utaratibu wa awali:
 - ✓ ***tunaokolewa kwa Imani pekee.***
 - Sheria inaweza kutuhukumu tu. Haiwezi kutuokoa kabisa.
- ❖ **Sheria na dhambi. Warumi 3:20.**
 - Sheria haikutimiza ahadi na haiwezi kutuokoa. Sasa nini kusudi lake?
 - Hutuonesha tunachopaswa kufanya na yakuacha kufanya ili kuepuka kumtenda Mungu dhambi. Tunaweza kuondoa dhambi kwa kuondoa sheria?
 - Katika kadhia hii, Kristo asingekufa kwa ajili yetu. Kama sheria inaweza kubatilishwa basi kafara isingehitajika.
 - Kuipuuza sheria hakufanyi kuua au kudanganya kusiwe dhambi tena.
 - Sheria ni ufunuo wa mapenzi ya Mungu yatokayo katika tabia yake. Kwa hiyo, Haiwezi kubadilika wala kuondolewa.